**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/NZ/2024/23**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000157**

**CORNELY JANUARY ............................................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO).........................MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 12 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 12 mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) (Mlalamikiwa) amrejeshe Mlalamikaji katika kundi la wateja wa matumizi madogo ya umeme ya chini ya uniti 75 (D1) kufuatia kumhamisha bila kuzingatia matumizi yake kinyume na Agizo la Bei . Bw. Nuwagi Mathias Karengi (Mwakilishi wa Mlalamikaji) anaeleza zaidi kuwa, yeye ni mkazi wa Kijiji cha Managhati kilichopo Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara hivyo anastahili kuwa katika kundi la matumizi madogo ya umeme.

Mlalamikaji alifanya jitihada za kutafuta suluhu kwa kufika ofisi ya Mlalamikiwa lakini malalamiko yake hayakuweza kupatiwa ufumbuzi hadi alipoamua kuwasilisha malalamiko yake katika Ofisi ya EWURA Kanda ya Kaskazini na kuiomba Mamlaka

(EWURA) kumuamuru Mlalamikiwa amrejeshe katika kundi la wateja wa matumizi madogo ya umeme.

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 10 mwezi Julai 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 31 mwezi Oktoba 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kubainisha kwamba Agizo la Bei la TANESCO la mwaka 2016 na mapitio yake ya mwaka 2020, bado halijakidhi matakwa ya kisheria kwa kuwa anaona kuna mapungufu kadha wa kadha, na hivyo anashikilia msimamo wa kumhamisha Mlalamikaji katika kundi la wateja wa matumizi madogo (D1) na kumpeleka katika kundi la wateja wa matumizi ya kati (T1) kwa kuwa mteja anaishi mjini.

Baada ya kupokea utetezi huo, Mamlaka (EWURA) ilipanga kikao cha usuluhishi tarehe 24 mwezi Januari 2025, wilayani Babati, ambapo Mlalamikaji hakufika na badala yake alituma ujumbe mfupi wa simu kuomba kuyaondoa malalamiko yake na kwamba hana nia ya kuendelea nayo kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wake.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 12 mwezi wa Februari 2025.

..............................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**